Cultural Orientation Resource Exchange

Congolese-Swahili Version

RASILIMALI KWA WAKIMBIZI





Photo: **E. Fichtner/IRC**

# Wakimbizi kujuwa Teknolojia Numerali (Technologie Numérique).

Teknolojia Numerali (Technologie Numérique) imebadirisha namna watu wanaishi mu duniya nzima. Itakuwa ya lazima piya mu maisha yako hapa Amerika, hata ikiwa hauzoweye kompyuta na Internet. Kujuwa bitu bya kawaida kuhusu Numerali (Numérique) na kujuwa hatari na piya bifaa bya Numerali (Numérique) itakusaidiya kupata habari na misaada fulani kwa usawa wakati unahamishwa na kukaa hapa.

## TEKNOLOJIA NUMERALI (TECHNOLOGIE NUMÉRIQUE) INATUMIKISHWA SAANA

Hapa Amerika, teknolojia numerali (Technologle Numérique) inatumikishwa mu shuruli (Activités) mengi tafauti. Itaweza kusaidiya kutafuta na kuomba kazi, kulipa factures na kupangiya pesa za umeweka mu banque, kufatililiya ma kazi zako na kufatililiya byenyi kupitikana ku masomo ya mtoto wako, kupata habari na misaada zenyi kupewa na serkali ao shirika zingine. Wanainchi wa Amerika wengine wanatumikisha Teknolojia Numérali kwa kuhemeya, kwa kulinda afya, kujifunza bitu bya mupya, na kujiburudisha (kujifurahisha). Na hizo shuruli zote zenaweza fanyika ku internet ukitumikisha kompyuta, ao simu, ao tablette.

## UPEKEE (VIE PRIVÉE)

Tunaweza sema kama, Internet iko kama masanga njiya kubwa ao soko. Ukienda ako, watu wanaweza kukuona na kuangaliya unafanya nini. Hiyo inawezakana isikuwe kitu kibaya; mu soko, ikiwa uko natafuta viyato vya sandales, mchuruzi anaweza akuone na anakupatiya sandales nzuri ku beyi ya chini. Watu, ao ma kampuni, wanaweza fanya piya bitu kama hibyo ku internet; banaweza chukuwa habari zako kuhusu shuruli (Activités) zako ku internet na batauzishiya habari zako ma kampuni zenyi kufanya publiscité, na batauzishiya ma kampuni zenyi kutaka kukuuzishiya kitu fulani...Ufundi fulani za mupya ku byombo bya numerali zinapewa na zina ruhusu benyi kubitumikisha kulinda usawa wa habari zako za upekee ku internet.

WAKIMBIZI KUJUWA TEKNOLOJIA NUMERALI







## USAWA (SECURITÉ)

Teknolojia numerali (Technologie Numérique) inatuwezesha bitu mingi saana na inatupatiya uwezo wa ajabu wakupata habari za lazima saana. Alakini, inaleta piya hatari za mupya kuhusu usawa na unaweza taka kuzijuwa ili ulinde habari zako za unafsi na upekee wako.



Simu nyingi ao byombo bingine bya namna hiyo unaweza bifunga ukitumikisha code ya securité ao alama ya kidole chako (Empreinte digiale). Kufunga (Ku bloquer) chombo yako ili batu benyi haujuwe basipate habari zako zenyi umeweka ku chombo kama,vkwa mfano ma photos, email ao byenyi kuwa ndani ya habari, piya basijuwe habari zako kuhusu compte ya banque yako.

Mara nyingi kutumikisha comptes zako za internet unaitaji kuwa na jina fulani ulioyo chaguwa (Nom d'utilisateur) (mara nyingi ni email yako) na neno la siri (mot de passe) na hibyo binaongeza usawa zaidi. Hiyo inazuwiya ba mwizi ba ku internet basiweze kuingiya ndani ya comptes zako na kupata habari zako. Wafundi wa usawa wa internet wanashahuriya batu basitowe neno la siri (mots de passe) kwa batu benyi haujuwi ao hauaminiye. Na banashahuriya piya usitumikishe hiyo neno moja ya siri (mots de pass) kwa kila compte. Wafundi piya wanaomba usiruhusu watu haujuwe ao hauaminiye kutumikisha simu (telephone) yako.

Saa zingine, unaweza taka kutumikisha kompyuta yenyi watu wengine wanaruhusiwa kutumikisha ao inawezekana muko wengi wenyi kutumikisha kompyuta. Kwa mfano ma bobliothèques nyingi hapa Amerika zinaruhusu watu wote kutumikisha kompyuta na internet bila kulipa. Ikiwa unatumikisha kompyuta ya watu wote, alakani, ni lazima ujuwe namna ya kufunga kipindi (session) yako ili kusikuwe habari zako zenyi kubaki mu kompyuta. Mara nyingi banapana hizo shahuri ao kutakuwa mtumishi wa bibliothèque mwenyi anaweza kukusaidiya.

## WATOTO NA INTERNET

Internet inapatiya Watoto mawezo (Opportunités) za namna mingi kuhusu masomo na jami (social). Wataitaji kujuwa namna ya kutumikisha teknolojia numerali (Technologie numérique) ili baendeleye ku masomo na baendeley muzuri mu maisha yabo. Watoto piya wanaitiajika kufunzwa kukuwa na hekima kuhusu kuonesha watu wengine ma picha zawo ao habari zao, namna gani banaweza tumikisha muzuri wakati yabo na habari zabo wakiwa ku internet, na namna gani kulinda upekee (vie privée) na habari zabo.

Byombo bingi bya numerali (digital) na Wi-Fi binapatiya wazazi uwezo wakufatililiya watoto, na wazazi wanaitajika kujuwa hiyo uwezo na kuitumikisha kwa kufatililiya byenyi batoto banafanya ku internet.



Photo: **Meredith Hutchison/IRC**

## BEYI YA KUTUMIKISHA SIMU NA DETA (MEGA)

Simu ya mkono inafanya kuwa kwepesi zaidi kukuwa nasumuliya na marafiki na ba ndugu, hata bakiwa mbali. Hapa Amerika, watu wanauza abonnement za simu zenyi kuruhusu kusumuliya, kutuma messages (SMS), na kupewa ma mega, byote pamoja ku beyi fulani kwa mwezi. Na beyi ya hizo abonnements zinafatana na simu ngapi unataka, utazitumukisha kiasi gani, na utazitumikisha namna gani. Kufanya bitu bingine, sawa kutuma emails, inatumikisha ma mega kidogo saana, alakini kufanya bitu bingine sawa kuangaliya ma videos, kusikiliza musique, ao kutuma ma photos inaweza tumikisha ma mega za mingi, na hiyo inaweza ongeza facture ya kutumikisha simu zaidi saana. Ukiwa na watu wengi wenyi kutumikisha simu na kompyuta nyumbani mwako, ni lazima ufatililiye namna gani batu unakaa nabo banatumikisha ma mega (deta) na ujuwe pesa ngapi unataka tumikisha. Unaweza piya amuwa kuuza bouquet yenyi kuwa na mega (deta) ao connection WI-FI wakati yote.

## BIFAA BYA NUMERALI (NUMÉRIQUE) KWA WAKIMBIZI

Ikiwa unataka kuangaliya habari zenyi kuwa ku internet kuhusu kuhamishwa na kukaa hapa Amerika na habari kuhusu Uongozi wa Mila na Tabiya, unaweza piya ingiya mu navigateur ya website ya habari za kuahamisha na kukaa za CORE (**https://corenav.org/**).

Ao chukuwa habari kutokeya ubao wa *Settle In* na hiyo unaweza ipata hapa: **https://corenav.org/en/settle-in/**.




Ikiwa unataka kujuwa zaidi kutumikisha byombo bya numérali (Numérique) na kujuwa kulinda habari zako za upekee wako, uulize watu wa kazi wa ofisi ya Kuhamishwa na kukaa kuhusu masomo ya numerali (Internet na bingine) yenyi inaweza kuwa karibu na fasi unayo ishi.

**Cultural Orientation Resource Exchange**
8719 Colesville Road, 3rd Floor • Silver Spring, MD 20910
For more information, visit the CORE Resettlement Navigator website at **corenav.org**.

Cultural Orientation Resource Exchange

The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**